

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



TAKUKURU KAGERA YAREJESHA JUMLA YA SHILINGI MILIONI KUMI NA NANE (KWA WASTAAFU KUTOKANA NA MIKOPO UMIZA,

TAARIFA KWA UMMA

JANUARI 16, 2021

1.0 Utangulizi

Ndugu wanahabari, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Kagera tumeendelea kutekeleza majukumu yetu kama yalivyoainishwa katika Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sheria namba 11 ya mwaka 2007. Katika utekelezaji wa majukumu yetu tumeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wa mapambano dhidi ya Rushwa wakiwemo waandishi wa habari, viongozi wa serkali na wananchi kwa ujumla.

Ndugu wanahabari,

TAKUKURU Mkoa wa Kagera mwanzoni mwa mwaka 2019 ilipokea taarifa kutoka kwa watumishi wastaafu watano ambao walikuwa wanamlalamikia **Bw. Marwa Machera** ambaye ni Msimamizi wa Kampuni ya **ANNY CREDIT CO LTD** kampuni ambayo inajishughulisha na shughulili za ukopeshaji wa fedha kwa wananchi mbalimbali katika

Wilaya ya Karagwe. Malalamiko ya wastaafu hao yalidai kuwa mtajwa aliwakopesha fedha kidogo lakini baada ya wastaafu kupokea mafao yao amechukua kiasi kikubwa cha fedha kwa kutumia vitisho.

Ndugu wanahabari,

Ufuatiliaji uliofanywa na TAKUKURU mkoa wa Kagera umeweza kubaini kuwa **Bw. Marwa Machera** ni Msimamizi wa Kampuni ya **ANNY CREDIT CO LTD** ambayo inafanya shughuli zake katika Wilaya ya Karagwe na kwamba shughui inazofanya ni za ukopeshaji wa fedha kwa watu mbalimbali wakiwemo wastaafu na amekuwa akifanya shughuli hizi za ukopeshaji tangu mwaka 2012 katika Wilaya ya Karagwe, na kwamba miongoni mwa watu aliowahi kuwakopesha wapo pia wastaafu watano ambao aliwakopesha kiasi tofauti tofauti kwa nyakati tofauti kati ya mwaka 2017 na 2018

Ndugu wanahabari,

Ufuatiliaji wetu umebaini kuwa wastaafu waliokopesha fedha ni kama wafuatao;-

- a) Chrispin Christian alikopesha shs 6,000,000/= mwaka 2017, Aprili. (Ambaye alirejesha shs 18,000,000/=)
- b) Benetson Ngambeki aliyekopesha shs 5,000,000/= mwaka 2018, Septemba (Ambaye alirejesha shs 16,120,000/=)
- c) Florida Damiani aliyekopesha shs 6,000,000/=mwaka 2017, Julai (Ambaye alirejesha shs 18,000,000/=)

- d) Revelian Rukonge aliyekopa shs 4,350,000/= mwaka 2017, Disemba (Ambaye alirejesha shs 21,150,000/=)
- e) Augustie Yohana aliyekopeshwa shs 15,000,000/=mwaka 2017, Aprili. (Ambaye alirejesha 48,300,000/=)

Ndugu wana habari,

Ufuatilaji wetu umebaini kuwa pamoja na kukopeshwa kiasi hicho cha fedha lakini mara baada ya wastaafu hawa kupokea mafao yao **Bw. Marwa Machera** aliwadai kiasi tofauti na kuwalazimisha kumlipa kiasi kikubwa zaidi tofauti na makubaliano yao hali iliyowafanya wastaafu hawa kukubali kulipa na kisha waliamua kutoa taarifa katika ofisi yetu ili kuweza kusaidiwa

Ndugu wanahabari,

Leo Tunawakabidhi wastaafu hawa sehemu ya fedha zao walizolipa kinyume ya taratibu kama ifuatavyo;-

- I. Chrispin Christian ambaye tunamkabidhi shs 3,000,000/= ambapo awali alikabidhiwa shs 2,000,000/= mwezi machi 2019 hivyo jumla amelipwa shs 5,000,000/=
- II. Benetson Ngambeki ambaye tunamkabidhi shs 3,000,000/= ambapo awali alikabidhiwa shs 2,000,000/= mwezi machi 2019 hivyo jumla amelipwa shs 5,000,000/=
- III. Florida Damiani ambaye tunamkabidhi shs 3,000,000/= ambapo awali alikabidhiwa shs 2,000,000/= mwezi machi 2019 hivyo jumla amelipwa shs 5,000,000/=

IV. Revelian Rukonge ambaye tunamkabidhi shs 4,000,000/= ambapo awali alikabidhiwa shs 2,000,000/= mwezi machi 2019 hivyo jumla amelipwa shs 6,000,000/=

V. Augustie Yohana ambaye tunamkabidhi shs 5,000,000/= ambapo awali alikabidhiwa shs 2,000,000/= mwezi machi 2019 hivyo jumla amelipwa shs 7,000,000/=

Hivyo leo tumekabidhi Jumla ya shs 18,000,000/= kwa wastaafu watano ambao awali walikabidhiwa shilingi 10,000,000/=. Jumla wamekabidhiwa shilingi 28,000,000/=

WITO

Tunatoa wito kwa wananchi wote kushirikiana na TAKUKURU na Serikali kwa ujumla katika mapambano dhidi ya Rushwa kwani Rushwa husababisha uvunjifu wa haki za binadamu na kumong'onyoa imani ya Wananchi kwa Serikali yao pia hudhoofisha maendeleo.

Niwaombe wananchi wenzangu kujjepusha nah ii mikopo umiza kwani ni chanzo kikibwa cha umaskini na pia inaweza ikasababisha mafarakano miongoni mwa jamii.

Imeandaliwa na

SIGNED

JOHN K.E JOSEPH

Mkuu wa TAKUKURU MKOA

